UFUATILIAJI WA UWAJIBIKAJI JAMII KATIKA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU

Taarifa ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii katika sekta ya Misitu, Wilaya ya Lindi 2015/2016

November 2015

Yaliyomo

Orodha ya Vifupisho 2

1.0 UTANGULIZI 3

1.1 KAMPENI YA MAMA MISITU 3

1.2 MAFUNZO JUU DHANA YA UWAJIBIKAJI JAMII 3

1.2.1 Mafunzo Juu ya Zana za Ufuatiliaji Uwajibikaji Jamii 3

1.3 MATOKEO YA UCHAMBUZI 4

1.3.1 Mpango na Mgawanyo wa Rasilimali. 4

1.3.2 Usimamizi wa Uadilifu 7

1.3.3 Usimamizi wa Utendaji/Uwajibikaji 7

2.0 TAARIFA YA MIKUTANO KATI YA KAMATI ZA MALIASILI, UONGOZI WA KIJIJI NA WANAJAMII 8

2.1 KIJIJI CHA MIHIMA 8

2.2 KIJIJI CHA NNDAWA 9

2.3 KIJIJI CHA MKANGA MOJA 10

3.0 VISA MKASA/SHUHUDA TOKA KWA WAJUMBE WA KAMATI ZA MALIASILI ZA VIJIJI 12

4.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA JUMLA 14

Orodha ya Vifupisho

DFO	District Forest Officer
GF	General Fund
H/W	Halmashauri ya Wilaya
JET	Journalist Environment Association of Tanzania
LEAT	Lawyers Environment Action Team
MJUMITA	Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania
MKUHUMI	Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ya Ukaa Kutokana na Ukataji na Uharibifu wa Misitu
MTEF	Medium Term Expenditure Framework
PF	Policy Forum
SAM	Social Accountability Monitoring
TFCG	Tanzania Forest Conservation Group
TNRF	Tanzania Natural Resource Forum

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 KAMPENI YA MAMA MISITU

Kampeni ya mama misitu ni kapeni ya mawasiliano ya miaka mitano yenye lengo la kuboresha utawala bora katika sekta ya misitu Tanzania na kuongeza uvunaji halali wa mazao ya misitu ili wananchi wazidi kunufaika kutokana na usimamizi endelevu wa misitu. Wadau katika kampeni ya Mama Misitu ni TRAFFIC, TFCG, MJUMITA, MCDI, FEMINA-HIP, Policy Forum, JET, LEAT, IGN-K na halmashauri ya wilaya ya lindi.

Kampeni ilianza mwaka 2014 baada ya makubaliano ya awamu ya pili kati ya wadau wa Mama Misitu na Jumuiko la Maliasili Tanzania baada ya makubaliano hayo , wadau wa kampeni walijitambulisha na kuitambulisha kampeni kwa kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lindi. Katika awamu hii ya kampeni ya Policy Forum ina jukumu la kutoa ujuzi katika mafunzo ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii kwa kipindi chote cha ufuatiliaji

1.2 MAFUNZO JUU DHANA YA UWAJIBIKAJI JAMII

Policy Forum kwa kushirikiana na MJUMITA kupitia Kampeni ya Mama Misitu walitoa mafunzo ya Uwajibikaji kwa Jamii yaani Social Accountability Monitoring (SAM) ikiwa na lengo la kuwawezesha wadau katika dhana nzima ya nini maana ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii katika mukutadha wa utoaji huduma kwa misingi ya Haki za Binadamu kupitia hatua kuu tano ambazo ni Mpango na Mgawanyo wa Rasilimali, Usimamizi wa Matumizi, Usimamizi wa Ufanisi/Utendaji, Uadilifu wa Umma na Usimamizi wa Uwajibikaji/Utendaji. Mafunzo ya uwjibikaji wa jamii yalilenga kuwawezesha wananchi kufanya uchambuzi juu ya mipango na bajeti ya halmashari hususani katika sekta ya Maliasili na Misitu ikiwa na kusudio la kuangalia kama utoaji wa huduma ulizingatia misingi ya haki za binadamu.

1.2.1 Mafunzo Juu ya Zana za Ufuatiliaji Uwajibikaji Jamii

Baada ya wadau kupata mafunzo juu ya dhana ya uwajibikaji jamii, wadau pia waliwezeshwa juu ya Zana za Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii, madhumuni ya mafunzo haya yalikuwa ni kuwawezesha wadau kuwa na ufahamu wa jinsi gani ya kuchambua nyaraka mbalimbali za serikali za mipango, bajeti, fedha na utekelezaji wa mipango/miradi katika kufuatiliaji uwajibikaji.

Mafunzo hayo yalijumuisha jumla ya washiriki 17 kati yao wanawake wakiwa 3 na wanaume wakiwa 14 kutoka katika makundi mbalimbali kama vile wenyeviti wa vijiji, watendaji wa vijiji, maafisa misitu, maafisa maendeleo jamii, wajumbe wa kamati za maliasili, asasi za kiraia katika ngazi za msingi/jamii, maafisa mipango, shirika lisilo la kiserikali wilaya ya Kilwa na waandishi wa habari wa magazeti na radio jamii mkoa wa Lindi

Baada ya mafunzo hayo, iliundwa timu ya kufanya uchambuzi. Uchambuzi ulifanyika baada ya kupata Mpango wa Halmashauri wa mwaka 2011/12-2015/16, Medium Term Expenditure

Framework (MTEF) pamoja na mihutasari ya vikao vya baraza la madiwani. Pia timu ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo Ndogo za Usimamizi wa Misitu Vijijini.

1.3MATOKEO YA UCHAMBUZI

1.3.1 Mpango na Mgawanyo wa Rasilimali.

Katika hatua hii ya Mfumo wa uwajibikaji jamii; uchambuzi hufanyika ili kuangalia ni kwa jinsi gani watoa huduma waliweza kupanga kulingana na mahitaji ya wananchi kwa kuzingatia vipaumbele vyao na pia walichambua mgawanyo wa rasilimali unaopelekea kufikiwa kwa mahitaji hayo.

Katika kufanya uchambuzi wa Mpango wa Halmashauri ya Lindi, timu ilibaini yafuatayo;

Muundo wa mpango; Muundo wa mpango umeandaliwa vizuri kwa muonekano wa rangi pamoja na mpangilio mzuri wa yaliyomo. Pia ilibaini **Malengo makuu H/W ambayo ni** kuboresha huduma za afya, elimu ya mafunzo ya mazingira , kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo na ufugaji , kuboresha huduma ya maji safi na salama na usimamizi wa maliasili.Ambapo kwa upande wa maliasili H/W ilipanga;

- *Kuhakikisha uwepo wa uboreshaji endelevu wa maliasili*
- *Kutoa elimu ya usimamizi wa misitu*
- *Kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi*
- *Kuongeza idadi ya doria za misitu*
- *Idadi ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kuongezeka.*

Pia timu iligundua kuwa, kulikuwa na ushahidi wa uchambuzi wa mahitaji (Chanzouk 4). Licha ya hivyo timu ilibaini kuwa kwa upande wa Rasilimali watu, Halmashauri haina uhakika kwani haioneshi idadi ya ongezeko la watumishi ifikapo 2016 (jedwali ukurasa wa 32)

Mgawanyo wa Rasilimali; Katika uchambuzi wa MTEF timu ilibaini kuwa jumla ya bajeti ya Halmashauri ilikuwa ni Tsh 17, 592,292,200

Jumla ya Bajeti	Mishahara	F/Maendeleo	Mapato Mengineyo	GF	Mapato ya Ndani
17,591,292,200.	10,201,597,000	4,536,916,900	1,961,487,300	225,595,000	638,696,000.



Katika bajeti kuu ya Halmashauri, Bajeti ya Malialisi ilikuwa ni Tshs**37,030,000 sawa na 4.75%** tu ya bajeti yote. Kwango hiki ni kidogo sana kwa ajili ya kitengo cha maliasili kama eneo moja wapo la kipaumbele katika mipango ya jumla ya halmashauri.

Uelewa mdogo kuhusu taratibu za uvunaji katika msitu wa hifadhi ya kijiji, hii inasababishwa na Afisa Misitu Wilaya kukosa fungu la bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuijengea uwezo jamii pamoja na kamati za maliasili juu ya umuhimu wa kuhifadhi misitu.

Pamoja na umuhimu wa Sekta hii ya maliasili katika kuchangia mapato ya ndani ya Halmashauri, bado inaonesha kitengo hicho kutopangiwa bajeti ya kutekeleza shughuli zake. Na hili lilidhihirika pale ambapo timu ilifanya vikao pamoja na kamati za maliasili, uongozi wa vijiji na wananchi katika vijiji vyenye hifadhi ya misitu ya kijiji. Moja ya Changamoto ziliozainishwa ni uelewa mdogo wa wananchi na kamati za maliasili juu ya taratibu za uvunaji katika misitu ya hifadhi ya vijiji. Na utoaji wa elimu hii ni jukumu la Afisa Misitu wilaya kulitekeleza, lakini anakwamishwa na kutokuwa na fungu maalumu la kumuwezesha kuvitembelea vijiji hivyo mara kwa mara kwa ajili ya kutoa elimu ya usimamizi na ufuatiliaji shirikishi wa misitu. .

Hivyo timu inashauri idara hii iweze kutengewa fungu la kutosha kwa ajili ya kumuwezesha Afisa Misitu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi na hii itasaidia katika kuboresha usimamizi wa misitu kwa kuzuia uvunaji haramu na kisha kuifanya misitu kuwa endelevu kwa manufaa ya sasa na ya vizazi vijavyo

Taarifa Nyinginezo

Baada ya timu kufanya uchambuzi wa Mpango Mkakati na MTEF, waliweza pia kufanya uchambuzi wa taarifa kama, *Muhtasari wa vikao vya Madiwani, Mpango wa uvunaji wa misitu*

(Miti) inayovunwa kwenye misitu huria ndani ya ardhi ya kijiji kwa mwaka 2010/2011 na 2015/2016 pamoja na *Sheria ndogondogo za uvunaji katika vijiji*

Mpango wa uvunaji wa misitu 2010/2011 na 2015/2016

Katika kufanya uchambuzi timu ilibaini yafuatayo;

a. Mabadiliko katika mpango wa uvunaji wa Wilaya
   - **Mwaka 2010/2011** : Tarafa za uvunaji zilikuwa sita (6)
   - **Mwaka 2015/2016** :Tarafa za uvunaji zilikuwa nane (8)
   - **Mwaka 2015/2016**: Tarafa za uvunaji zimeongezekwa kutokana na mahitaji. Pia katika mipango yote miwili tumegundua kuwa tarafa ya Ng'apa, Nangalu na Milola hazipo kwenye mpango wa uvunaji wa wilaya kwa vile kuna mradi wa majaribio wa MKUHUMI hivyo maeneo hayo hayaruhusiwi kwa uvunaji

b. Changamoto za utelekezaji wa Mpango wa Uvunaji

   a) Wateja wengi wanapendelea kuvuna miti ambayo ina soko wakati miti ipo mingi mfano mipingo , mninga n.k. Ofisi inatatua tatizo hilo kwa kugawa kiwango cha uvunaji kwa kuzingatia uwezo wa mita za ujazo zilizotengwa kwa mwaka huo
   b) Hakuna tathmini ya kitaalamu inayofanyika katika mapori ya uvunaji kwa kila mwaka ili kubaini kiwango na aina ya miti iliyotayari kuvunwa. Ufumbuzi-Tunategemea taarifa kutoka kwa wavunaji baada ya kutembelea mapori pamoja na , viongozi wa vijiji na watendaji.
   c) Uvunaji haramu pia ni changamoto kubwa katika kutekeleza mpango wa uvunaji. Hivyo tunapendekeza uwepo wa doria za mara kwa mara na serikali za vijiji kusimamia rasilimali za misitu katika maeneo yao.

c. Uendelevu wa miti inayovunwa

   Kutokana na kutokufuatwa kwa taratibu za uvunaji wa mazao ya misitu, uendelevu wake upo katika hali ya kupunguwa au kutoweka kabisa kwa sababu mapori huria si tu hayana mpango wa uvunaji tu bali hayana mpango wa usimamizi pia hivyo yanategemea usimamizi na doria hafifu kutoka kwa serikali za vijiji kupitia kamati za maliasili za vijiji. .

   Taarifa hii inapatikana katiika vitabu vya mpango wa uvunaji wa mwaka 2010/2011 (uk 10-12) na mpango wa uvunaji wa mwaka 2015/2016 (uk 10-12).

Mapato na Mgawanyo

Mapato na mgawanyo wa fedha zitokanazo na uvunaji yamegawanyika katika makundi mawili katika ngazi ya vijiji, ambapo kundi la kwanza ni asilimia 60% ya mapato hupelekwa kwa kamati ya maliasili na asilimia 40% hupelekwa katika Serikali ya kijiji.

1.3.2 Usimamizi wa Uadilifu

Katika kufanya uchambuzi wa taarifa ya madiwani, timu ilibaini kuna hatua za kinidhamu ambazo zilichukuliwa dhidi ya watumishi walioenenda kinyume na utaratibu. Mfano Baraza la Madiwani lilimuagiza Mkurugenzi wa halmashauri amchukulie hatua za kinidhamu Mtumishi aliefanya uzembe katika usimamizi wa ujenzi wa barabara ya mipingo – mnyangara ambapo alishushwa cheo kutoka kuwa kaimu Mhandisi ujenzi (W) na kuwa mhandisi wa kawaida wa daraja la II. Pamoja na adhabu hiyo, Baraza lilimuagiza Mkurugenzi afanye utaratibu wa kumuhamisha mtumishi huyo kwani wananchi pamoja na baraza hilo hawakuwa na Imani naye tena. *(Chanzo; Masuala ya watumishi uk9-10 – Muhtasari wa Kikao cha Baraza la Madiwani)*

1.3.3 Usimamizi wa Utendaji/Uwajibikaji

Katika hatua hii ya uchambuzi, timu iligundua kuwa baraza la Madiwani hupitia hoja za mkaguzi mkuu wa hesabu za Serikali na kuiagiza halmashauri kuzingatia mapendekezo na hoja zilizotelewa na mkaguzi. Mfano katika muhtasari wa kikao maalum cha tarehe 19/10/2013 uk 3kum no 15/2013/2014, baraza liligundua kuwa kuna baadhi ya hoja ambazo halmashauri walizitolea maelezo lakini kikao hawakuridhika nayo na hivyo kuigiza tena halmashauri kufanyia kazi hoja hizo;

Mfano niutekelezaji wa miradi, kikao hakikuridhika na baadhi ya majibu ya hoja za ukaguzi kwani zimejibiwa bila kuwepo na ushahidi wa vielelezo. Pia hakikuridhika na hali ya kutotekelezwa kwa miradi ya kilimo yenye thamani Shs 535,892,500 hadi kufikia tarehe 30/06/2012. Hii ni kinyume cha kanuni za fedha za umma (makato na adhabu) za mwaka 2005

Hivyo kikao kilimuagiza Mkurugenzi Mtendaji ahakikishe maafisa ugani wote wanatengeneza ratiba maalum itakayoonyesha namna watakavyo tembelea katika maeneo yao kutimiza shughuli za kilimo na wawe na muongozo wa kazi.

Vilevile katika muhtasari maalum wa Baraza la Madiwani tarehe 28/08/2014 uk1, kumb na 6/2014/2015, ripoti ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za fedha ya juni 30, 2013. Ripoti hiyo ilieleza kwamba katika mwaka wa fedha 2012/2013 halmashauri haikuonyesha kwenye kitabu cha hesabu mada 1 ambayo yangeweza kujitokeza ya tsh 197,923,870 kutokana na kesi ya Halmashauri mpaka kufika tarehe 30 june 2014. Halmashauri ilikuwa inadai jumla ya tshs 405,876,000 kuna wasiwasi wa ukusanyaji wa kiasi hicho kwani inaonekana kimekaa muda mrefu bila kukusanywa.

Hadi kufikia30 June 2013, H/W ilikuwa inadaiwa tshs 164,237,000 na deni hili ni la muda mrefu. Vilevile halmashauri ilikuwa ina jumla ya mapato ya kiasi cha tshs 11,016,111 ambayo yalikusanywa lakini hayakupelekwa benki. Ikiwa ni kinyume na memoranda ya fedha za serikali za mitaa mwaka 2010 na hakuna adhabu iliyotolewa kama inavyo elekeza katika kanuni za fedha za umma (makato na adhabu) za mwaka 2005

TULICHOJIFUNZA NA CHANGAMOTO

Upatikanaji wa taarifa; katika kutekeleza zoezi la uwajibikaji kwa jamii yaani SAM, nyenzo muhimu ni uwepo wa taarifa mbalimbali zinazowezesha kufanya uchambuzi, kwa upande wa

halmashauri ya Lindi, timu ilipata changamoto ya kupata taarifa zote na badala yake walipata baadhi tu ya taarifa na hivyo kushindwa kufanya uchambuzi katika hatua zote tano za mfumo wa uwajibikaji kwa jamii.

Kueleweka kwa taarifa na ubora wake; timu ilibaini kuwa ni vigumu kuelewa taarifa za halmashauri kwanza ni kwasababu ya lugha inayotumika ambayo ni kiingereza ambapo watanzania waliowengi wanaelewa Kiswahili. Vilevile ubora na uhalisia wa taarifa ni hafifu kwani kuna baadhi ya taarifa ziliandikwa kama mradi umekamilika kwa 100% lakini sehemu ya maoni inaonyesha mradi unaendelea.

SEHEMU YA PILI

2.0 TAARIFA YA MIKUTANO KATI YA KAMATI ZA MALIASILI, UONGOZI WA KIJIJI NA WANAJAMII

Baada ya timu ya SAM kufanya uchambuzi na kuandika ripoti ya awali, PF, MJUMITA, wataalamu wa misitu, pamoja na baadhi ya wanatimu walikutana na Kamati za maliasili, serikali ya kijiji pamoja na wanakijiji katika vijiji vilivyokuwa na misitu ya hifadhi inayovunwa na ile iliyopo katika mradi wa MKUHUMI. Lengo ikiwa ni kuangalia changamoto zinazoikabili sekta ya maliasili na misitu na jinsi ya kutatua changamoto hizo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

2.1 KIJIJI CHA MIHIMA.

Kijiji hiki kina msitu uitwao Mihima, Msitu huu ni wa hifadhi ya kijiji ulianzishwa mwaka 2001 na unaukubwa wa hekta 2662. Uvunaji wa kwanza ulianza mwaka 2013. Kamati ya maliasili ina jumla ya wajumbe 10 kati yao wanawake ni 3 na wanaume ni 7. Hata hivyo katika kipindi hiki kijiji kimekabiliwa na changamoto ya kiuongozi ambapo wanakijiji wamewatuhumu viongozi kushiriki katika shughuli za uvunaji haramu wa mazao ya misitu na kukisababishia kijiji hasara. Changamoto hii ilipelekea maazimio ya wanavijiji katika mkutano wa hadhara ambayo yalipitisha utenguzi wa halmashauri ya kijiji na kamati ya maliasili ya kijiji katika kipindi cha mwezi wa 11.

TULICHOJIFUNZA

- Uelewa mdogo kuhusu taratibu za uvunaji katika msitu wa hifadhi ya kijiji, hii inasababishwa na Afisa Misitu Wilaya kukosa fungu la bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ikiwemo kujengea uwezo jamii pamoja na kamati za maliasili juu ya umuhimu wa kuhifadhi misitu.
- Kutofuata taratibu za utunzaji wa fedha mfano kijiji kutopeleka fedha za uvunaji benki
- Uelewa mdogo kuhusu majukumu ya kamati ya maliasili hususani kwa wajumbe wapya wa kamati hiyo. na hii inasababishwa nakutokubakiza wajumbe wenye uzoefu kutoka katika kamati ya zamani
- Ushirikishwaji hafifu wa wanajamii katika kufanya maamuzi yanayohusu usimamizi wa misiti hivyo kupelekea kutoaminika kwa kamati hiyo mbele ya jamii.

- Ushiriki mdogo wa kinamama katika doria, hii inasababishwa na hofu ya majangili wanaokumbana nao katika doria, lakini pia na mfumo dume (hofu ya kuachwa na waume zao mara wanapokuwa kwenye doria za muda mrefu)
- Moto kichaa hasa kipindi cha kiangazi. Kumekuwa na tabia ya uchomaji wa misitu kulingana na mila na desturi
- Uvunaji haramuna usio endelevu na kuwepo kwa mashamba ndani ya hifadhi ya msitu, hii inasabinshwa na umaskini pamoja na jamii kutopata manufaa ya moja kwa moja ya msitu.

2.2 KIJIJI CHA NNDAWA

Kijiji hiki kina msitu uitwao Nndawa, Msitu huu ni wa hifadhi ya kijiji ulinzishwa mwaka 2002 na unaukubwa wa hekta 646. Kamati ya maliasili inajumla ya wajumbe 10 kati yao wanawake ni 5 na wanaume ni 5.

TULICHOJIFUNZA

- Uelewa mdogo kuhusu taratibu za uvunaji katika msitu wa hifadhi ya kijiji, hii inasababishwa na Afisa Misitu Wilaya kukosa fungu la bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ikiwemo
- Kukosekana kwa motisha kwa jamii kushiriki katika uhifadhi wa misitu mfano pamoja nakijiji kuwa na mpango wa uvunaji hakijaweza kutekeleza mpango huo.
- Kujengea uwezo jamii pamoja na kamati za maliasili umuhimu wa kuhifadhi misitu.
- Kutofuata taratibu za matumizi fedha mfano kutokuwepo uwazi katika matumizi ya fedha za uvunaji kiasi cha Sh mil 2, hivyo jamii kutokuwa na imani na kamati ya maliasili
- Uelewa mdogo kuhusu majukumu ya kamati ya maliasili hususani kwa wajumbe wapya wa kamati hiyo. na hii inasababishwa nakutokubakiza wajumbe wenye uzoefu kutoka katika kamati ya zamani
- ushirikishwaji hafifu wa wanajamii katika kufanya maamuzi yanayohusu usimamizi wa misititu hivyo kupelekea kutoaminika kwa kamati hiyo mbele ya jamii na ushiriki mdogo katika doria
- ushiriki mdogo wa kinamama katika doria, hii inasababishwa na hofu ya majabgili wanaokumbana nao katika doria, lakini pia na mfumo dume (hofu ya kuachwa na waume zao mara wanapokuwa kwenye doria za muda mrefu)
- Moto kichaa hasa kipindi cha kiangazi. Kumekuwa na tabia ya uchomaji wa misitu kulingana na mila na desturi
- uvunaji haramu na usio endelevu na pamija na matumizi ya chain saw katika upasuaji wa mbao hii inasabinshwa na umaskini pamoja
- Mwingiliano wa majukumu kati kamati ya maliasili na serikali ya kijiji. Mfano hii inatokana na ukosefu wa elimu juu ya uendeshwaji wa kamati za maliasili na serikali ya kijiji
- Masuala ya kisiasa kuingilia shughuli za uhifadhi wa misitu. mfano kijiji kililazimika kuvuna mbao kwa ajili ya maabara. Na uvunaji huo mbao zilipasuliwa kwa kutumia chain saw swala ambalo lilileta mgogoro mkubwa kwa jamii.

- Utekelezaji na usimamizi mbovu wa sheria ndogo za usimamizi wa misitu. Kamati na uongozi wa kijiji umekuwa ukiwasamehe wahalifu na kutofuata kanuni ya adhabu.

MAPENDEKEZO

- kujengea uwezo kamati za maliasili juu ya majukumu yao, usimamizi wa sheria ndogo pamoja na uwezo wa kuingia na kusimamia mikataba ya uvunaji wa wafanyabiashara
- Ushirikishwaji wa wajumbe wa kamati ya zamani katika kujengea uwezo kamati mpya
- Kuongeza uwazi na ushirikishwaji wa jamii katika doria na maamuzi yanayohusu uvunaji na uhifadhi wa misitu
- Kutangaza maombi ya wavunaji wapya katika msitu wa hifadhi. Hapa DFO amepata mvunaji mmoja na mkakati ni kuongeza idadi ya wavunaji ili kuleta ushindani.
- Kutenga fedha zitokanazo na uvunaji kwa ajili ya huduma za ugani, hii itamuwezesha afisa misitu kutoa huduma za ugani vijijini.
- kufanya mikutano ya vijiji ili kupanga vipaumbele vya maendeleo ili fedha zitokanazo na uvunaji wa misitu zisaidie shughuli za maendeleo kijijini
- Afisa maliasili afuatilie upatikanaji wa Nyundo kwa ajili ya misitu ya hifadhi ya vijiji
- Vijiji viangalie vipaumbele vya wilaya kabla ya kutekeleza miradi yao hii itapungua muingiano katika utekeleza
- Vijiji kupeleka taarifa za robo mwaka kwa DFO
- Kupitia mipango ya uvunaji katika hifadhi yamisitu ya vijiji ili kuendana na wakati. mfano kutozingatia bei elekezi kama inavotolewa na serikali. mfano vijiji vilikuwa bado vinauza mbao kwa bei ya chini kati ya 6000/= mpaka 8000/= ukilinganisha na bei elekezi ambayo ni 19,900/=
- Ofisi ya DFO kuongeza vitabu kwa ajili ya kutolea taarifa za doria

2.3 KIJIJI CHA MKANGA MOJA

Kijiji hiki kina msitu uitwao Mkanga moja ulio chini ya mradi wa MKUHUMI ambao ulianza 2010 na uzinduzi ulifanyika 2011. Msitu una ukubwa wa hecta 1541.45. Wajumbe wa kamati ya maliasili wapo 12 kati yao 4 ni wanawake na wanaume ni 8. Msitu huu una mpango wa usimamizi na sheria ndogo ambazo zimepitishwa na baraza la madiwani. Katika kutekeleza mpango wa majaribio wa MKUHUMI awamu ya kwanza kijiji kilipata jumla ya Shillingi millioni 8 ambazo ziligawanywa kwa wanakijiji wote na kila mwanakijiji alipata kiasi cha Shillingi 6500. Katika awamu ya pili Kijiji kilipata Sh. 14,000,000 ambapo kati ya hizi kijiji kiligawana sh 10,000,000 na kila mwanakijiji alipata Shilingo 10,000/= na kiasi cha shillingi 4,000,000/= zilipelekwa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ya kijiji.

TULICHOJIFUNZA

- Uelewa mdogo kuhusu taratibu za uvunaji katika msitu wa hifadhi ya kijiji, hii inasababishwa na Afisa Misitu Wilaya kukosa fungu la bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake

- Kukosekana kwa motisha kwa jamii kushiriki katika uhifadhi wa misitu mfano fedha za hewa ya ukaa kutoletwa kijiji kwa takribani miaka mitatu tangu mradi kuisha
- Kujengea uwezo jamii pamoja na kamati za maliasili umuhimu wa kuhifadhi misitu.
- Uelewa mdogo kuhusu majukumu ya kamati ya maliasili hususani kwa wajumbe wapya wa kamati hiyo. na hii inasababishwa nakutokubakiza wajumbe wenye uzoefu kutoka katika kamati ya zamani
- ushirikishwaji hafifu wa wanajamii katika kufanya maamuzi yanayohusu usimamizi wa misitu hivyo kupelekea kutoaminika kwa kamati hiyo mbele ya jamii na ushiriki mdogo katika doria
- ushiriki mdogo wa kinamama katika doria, hii inasababishwa na hofu ya majangili wanaokumbana nao katika doria, lakini pia na mfumo dume (hofu ya kuachwa na waume zao mara wanapokuwa kwenye doria za muda mrefu)
- Moto kichaa hasa kipindi cha kiangazi. Kumekuwa na tabia ya uchomaji wa misitu kulingana na mila na desturi
- uvunaji haramu na usio endelevu na pamija na matumizi ya chain saw katika upasuaji wa mbao hii inasabinshwa na umaskini pamoja
- Masuala ya kisiasa kuingilia shughuli za uhifadhi wa misitu. mfano kijiji kililazimika kuvuna mbao kwa ajili ya maabara. Na uvunaji huo mbao zilipasuliwa kwa kutumia chain saw swala ambalo lilileta mgogoro mkubwa kwa jamii.
- Mgogoro wa ardhi na mipaka ya kijiji jirani inayopelekea uvamizi na uvunaji haramu na hii imesababishwa na ushirikishwaji mdogo wa jamii katika kutambua mipaka
- Utunzaji mbovu wa kumbukumbu za kamati ya maliasili pamoja na serikali ya kijiji. hii imechangia kwa kamati mpya za maliasili kutokuwa na uelewa wa awali juu ya historia ya msitu wa hifadhi ya kijiji pamoja na majukumu yao.
- Utekelezaji na usimamizi mbovu wa sheria ndogo za usimamizi wa misitu. Kamati na uongozi wa kijiji umekuwa ukiwasamehe wahalifu na kutofuata kanuni ya adhabu.

MAPENDEKEZO

- Kujengea uwezo kamati za maliasili juu ya majukumu yao na usimamizi wa sheria ndogo
- Ushirikishwaji wa wajumbe wa kamati ya zamani katika kujengea uwezo kamati mpya
- Kuongeza uwazi na ushirikishwaji wa jamii katika doria na maamuzi yanayohusu uhifadhi wa misitu
- Kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi endelevu ya fedha zitokanazo na mradi wa MKUHUMI mfano wanajamii kuacha kugawana fedha badala yake wawekeze katika miradi ya maendeleo
- Kufanya mikutano ya vijiji ili kupanga vipaumbele vya maendeleo ili fedha zitokanazo na uvunaji wa misitu zisaidie shughuli za maendeleo kijijini
- Kuangalia upya suala la mipaka kati ya kijiji cha Mkanga moja na vijiji jirani

SEHEMU YA TATU: VISA MKASA/SHUHUDA TOKA KWA WAJUMBE WA KAMATI ZA MALIASILI ZA VIJIJI

3.0 VISA MKASA/SHUHUDA TOKA KWA WAJUMBE WA KAMATI ZA MALIASILI ZA VIJIJI

Rehema P. Mbwago, miaka 49, mjumbe wa serikali ya kijiji cha Miima kilichopo wilaya ya Lindi vijijini kwa sasa ni mjumbe wa kamati ya Maliasili .Nimefanya kazi ya kulinda msitu kwa muda wa miaka 13 wakati naingia kwenye kamati ya maliasili nilikuwa nina mtoto wa mwaka mmoja na nusu. Nilikubali kufanya kazi ya kulinda misitu kwasababu wakina mama ndiyo waathirika zaidi pale mazingira yanapokuwa yameharibiwa kuliko akina baba mfano wakina mama hufuata maji mbali pale vyanzo vya maji vinapoharibiwa. Wamama tukiwezeshwa kielimu, mafunzo ya vitendo kama vile ufuatiliaji na usimamizi wa Misitu, tunaweza bila tatizo. Hii ikiwa ni pamoja na kushiriki doria kama wakina baba wanavyoshiriki. Kila mwanajamii ana haki ya kusimamia mazingira, awe mwanamke ama mwanammme. Nikiwa kama mwanamke nipo tayari kusimamia mazingira.

Bakari B. Sale, miaka 45, Mkazi wa kijiji cha Mihima wilaya ya Lindi vijijini. Katibu wa kamati ya maliasili ambayo ni muanzilishi wa msitu wa hifadhi ya kijiji cha Mihima ambao ulianzishwa mwaka 2001. Kabla ya kuanzishwa kwa mradi huu hali ya uwajibikaji haikuwa nzuri, jamii haikuona umuhimu wa kutunza Misitu. Lakini baada ya kupata mafunzo mbalimbali yaliyotolewa na kampeni ya mama Misitu na mashirika mengine kama vile TFCG na MJUMITA, wanajamii ilianza kuona umuhimu wa kufuatilia na kusimamia rasilimali Misitu ijapokuwa bado haijakubali na kuamini kwamba kuna kitu kinachoweza kunufaisha jamii au kusaidia jamii. Nikiwa katibu wa kata ya Namupa ambayo inajulikana kama TUME YA JANA(Tunza Misitu ya Jamii ya Namupa), nilibahatika kupata mafunzo ya ufuatiliaji na uwajibikaji yaliyoratibiwa na kampeni ya Mama Misitu kwa kushirikiana na Policy Forum. Mafunzo yalinipa ufahamu mkubwa katika akili yangu. Nami nilitoa mrejesho kwenye mkutano wa hadhara na kuelimisha wanakijiji wenzangu na serikali ya kijiji katika kuhakikisha kwamba

kuna kuwa na uwajibikaji katika shughuli zote za misitu na mambo mengine ya kijiji. Jamii inahusika kwa karibu sana kuhakikisha tunapanga mipango kwa pamoja tunatekeleza kwa pamoja na ufuatiliaji wa pamoja ili kila mtu ajiridhishe kwa kila kinachofanyika kwa jamii na jamii itanufaika nacho.

Awali kulikuwa na changamoto, wanajamii hawajui mapato na matumizi ya serikali ya kijiji na kamati zake. Pia mikutano ya kusoma mapato na matumizi haikufanyika kwa takribani miaka miwili. Baada ya kuwapa elimu serikali ya kijiji imefanya mkutano wa mapato na matumizi na jamii sasa hivi imeshaanza kuona kwamba kweli swala la uwajibikaji limeshaanza kuonekana katika uongozi wa kijiji. Kwa sasa naona muamko baada ya kuja MJUMITA kupitia kampeni ya Mama Misitu kutoa elimu kwa serikali ya kijiji cha Miima na kamati ya maliasili. Kuna muelekeo mkubwa unaonesha uongozi kwa sasa utakuwa unawajibika zaidi kwa jamii ilikuepusha malalamiko ya mara kwa mara kwa kutumia fedha bila utaratibu

Juma M. Juma, miaka 49, Mkazi wa kijiji cha Nndawa kilichopo wilaya ya Lindi vijijini

Changamoto zilizopo hapa kijijini ni utofauti kati ya serikali ya kijiji na kamati ya kijiji hawaelewani kabisa taarifa hazitolewi kwa uwazi kutokana na hivyo mambo mengi hayafanyiki kwenye ukamilifu na hii inapelekea wananchi kushindwa kutambua na kushindwa kuelewa ni jinsi gani wanaweza kuwajibika kwa kuwa taarifa hazitolewi ipasavyo kwa wakati na muda husika .Ili tunufaike katika utunzaji wa misitu inatakiwa serikali na kamati yake iwe kitu kimoja katika kuweka mambo kwenye ukamilifu, uwazi na kuwajibika kwenye shughuli mbalimbali za hapa kijijini.

Mussa J. Makuwango, miaka 26, Mkazi wa kijiji cha Mkanga moja. Katibu wa kamati ya maliasili na sasa hivi ni mjumbe wa kijiji . Mwaka 2011 tulikuwa na mradi wa MKUHUMI tuliupokea vizuri na ulijumuisha vitongoji vyetu vyote vinne,lakini kabla ya mradi kuzinduliwa tayari tulikuwa na wawezeshaji kutoka wilayani walitusaidia katika uzinduaji wa mradi huu.Mtendaji na mwenyekiti walitusaidia kwenda kwenye kila kitongoji kuchukua maoni ili yaweze kufikishwa kwenye mkutano wa hadhara na kuweza kupata maamuzi ya pamoja,mwaka 2011 kamati ya maliasili

ilichaguliwa na kubainishwa kwenye mkutano wa hadhara wa kijiji na kamati hiyo ilianza kufanya kazi za doria.Changamoto tunazo kumbana nazo kwenye kamati hii ya maliasili ni uvamizi wa hifadhi yetu ya misitu kutoka vijiji jirani navyo ni Chikonji, Ng'apa na Kineng'ene kutokana na imani potofu ya vijiji hivyo ya kuwa wanadhulumiwa maeneo yao na sababu kubwa ya migogoro hii ni faida inayopata kijiji chetu kutokana na msitu wetu tumeweza jengewa ofisi na zahanati kutokana na hali hiyo vijiji jirani wanaingia kwenye misitu yetu na kufanya fujo ili Mkanga 1 wasiendelee kupata faida itokanayo na kuhifadhi misitu, mimi kama mwanakijiji kwa sasa ninaisaidia na nitaisaidia kamati ya kijiji kuhakikisha maeneo yetu yote ya hifadhi ya misitu yanakwenda vizuri na kutatua migogoro yote ya maeneo yanayotuzunguka kama Chikonji walituvamia kwenye eneo letu kwakukata mbao kwa mashine ya 'cheni soo' ila kwa sasa hali imetulia kwasababu ya doria za kila siku zinafanyika, na upande wa Kineng'ene wao wana mgogoro na kijiji cha Mkanga 1 kwasababu wanadai kuna eneo lao ambalo limechukuliwa na kijiji chetu hili tatizo ili litulie inabidi kwenda mara kwa mara kuzungumza na watu husika wa kijiji hicho na mpaka sasa mambo yanaendelea vizuri kidogo.Hivyo basi tunaiomba manispaa ya Lindi itusaidie kusuluhisha hii migogoro ya mipaka hapa kijijini kwetu Mkanga moja.

SEHEMU YA NNE: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

4.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

Ushirikishwaji wa wanajamii katika usimamizi wa misitu ni muhimu sana, hii itachochea wao kuona umuhimu pamoja na faidaya mali asili hiyo, kwani jamii inapopewa kipaumbele katika kufanya maamuzi yenye faida kwao inasaidia kuleta maendeleo endelevu. Vilevile katika taarifa hii tumeona kuna baadhi ya vijiji vyenye migogoro ya mipaka hivyo tunaishauri halmashauri ya wilaya ya Lindi kuweza kuishughulikia migogoro hiyo kwa haraka kwani kwa kiasi Fulani tumeona inachangia katika uvunaji haramu wa misitu. Jambo la mwisho lakini sio kwa umuhimu, tumegundua kuwa idara ya maliasili hutengewa bajeti finyu katika halmashauri, Hivyo timu inashauri idara hii iweze kutengewa fungu la kutosha kwa ajili ya kumuwezesha Afisa Misitu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi na hii itasaidia katika kuboresha usimamizi wa misitu kwa kuzuia uvunaji haramu na kisha kuifanya misitu kuwa endelevu kwa manufaa ya sasa na ya vizazi vijavyo.